

VIDOKEZO VYA MOFOLOJIA YA KITENZI KATIKA LUZINZA

Y.I. Rubanza

Idara ya Kiswahili, Chuo kikuu cha Dar es Salaam

Ikisiri

Lengo la makala hii ni kutoa maelezo mafupi ya sarufi ya lugha ya Luzinza ikizingatiakipengele cha mofolojia ya kitenzi. Huu utakuwa mwanzo wa kuchochea uandishi wa kina wa sarufi ya lugha hii. Mfuatano wa viambishi (mofimu) mbalimbali vinavyounda kitenzi umeelezwa ukijumuisha mofimu tangulizi, mzizi, na mofimu fuatishi, yaani mofimu nyambulishi za kitenzi. Aidha kipengele cha kutengamana kwa mofimu kimeelezwa kwa kuzingatia minyambuliko ya vitenzi vya silabi moja na silabi zaidi ya moja. Pametolewa pia maelezo mafupi na mifano ya dhana ya uradidi wa mizizi; na vielelezo vya mofimu zinazonyambuliwa kutokana na nomino na maneno mengineyo. Makala hii inahitimishwa na maelezo mafupi ya vipengele ambavyo havikuguswa (kutokana na ufinyu wa makala yenyewe) ili vielezwe kwa kinagaubaga na watafiti wengineo.

1.0 Utangulizi

Luzinza ni lugha mojawapo ya lugha zipatazo 150 zinazozungumzwa nchini Tanzania (LOT 2009, Rubanza 2009). Inakadiriwa kuwa na wazungumzaji wapatao 187,105 (LOT2009) na hivyo kuwa lugha ya 46 kwa kuzingatia wingi wa wazungumzaji nchini. Kutokana na miainisho mbalimbali ya lugha iliyofanywa na wanaisimu kadhaa, kwa ujumla Guthrie (1948, 1967), Nurse (1979) na Nurse na Phillipson (1980) na wengineo, Luzinza ni lugha inayoangukia katika kundi la lugha E. 2. Miainisho hii ya lugha ya Luzinza imewekwa pamoja na lugha ya Lunyambo, (E.21) Luziba, Luhaya (E.22), Kerebe (E.24) na Jita (E. 25) (2009a). Aidha lugha hii Lugha hii inakaribiana sana pia na lugha ya Lunyankore na Lunyoro za Uganda. Inazungumzwa hasa katika maeneo ya Magharibi na kusini mwa Ziwa Victoria na baadhi ya visiwa katika ziwani). Inazungumzwa katika wilaya za Muleba, Biharamlo, Chato katika mkoa wa Kagera. Aidha lugha hii inazungumzwa pia katika wilaya za Sengerema, Geita mkoani Mwanza na katika wilaya za Kahama, Bukombe katika mkoa wa Shinyanga. Majina yatumikayo katika maandishi mbalimbali ya kiisimu ni pamoja na Echijinja, Echidzindza, ecizinza, Dzinza, Jinja, zinja, Dzindza, kizinza na Luzinza.

2.0 Mofolojia ya Kitenzi

Kiini cha kitenzi ni mzizi, ambao hufungamanishwa na viambishi awali na viambishi tamati (mofimu). Mzizi, kiambishi ku-, na irabu ya mwisho –a huunda kitenzi kisoukomo. Mifano inayohusika na dhana hiyo ni kama *ku-ombeka* (ku-jenga), *ku-runga* (ku-unga, kutia viuongo) *ku-nogola* (ku-kata) n.k. Muundo wa kitenzi cha kuamuru (kitenzi amuru) hudondosha ku- kama ioneshwavyo katika maneno ya mifano iliyotolewa hapo juu yaani; *yombeka* - jenga; *runga* – unga/tia viuongo; *-nogola* – kata; n.k.

2.1 Mfuatano wa mofimu katika muundo wa kitenzi

Katika lugha ya Luzinza kama, zilivyo lugha nyingi za Kibantu kuna mfuatano wa elementi katika kitenzi kama ifuatavyo: 1. kisabiki kiambishi awali; 2. kioneshi dhamira *ka-*, sharti *ki-* na mazoea *ni-*; 3. kikanushi *ti-*; 4. kinominishi; 5. kikanushi-*ta-*; 6. kioneshi njeo; 7. kioneshi yambwa; 8. kijirejee *-e*; 9. mzizi; 10. vinyambulishi vya kitenzi; 11. kitimilifu *-ir-*; 12. irabu ishilizi; 13. kiangamitamati; 14. njeo kiangamitamati-*ga*.

Jedwali la 1: Baadhi ya mfuatano wa viambishi katika kitenzi

1	2	3	4	5	6	7	8	9	10	11	12	13	
			a	ta		mu		kund		a			asimkubali
		ti	tu		ka			lim	ir	e			hatujalima
			ni			mu	ba	jum		a			mnawatukana
	ka		n	ta				sak		a			nisihemee (chakula)
		ti	n		ka			tek		a		ga	sijapika
			tu	ta		ku	m	tel		a			tusimpige
			ni			mu		gambil		a			ninamwambia
			tu		ka	mu		gay		a			tulimdharau
			a	ta		kwi		iz		a			asije
			a		ka	ba		gamb	ir	a			aliwambia
	ni		m			ba		yimb	ir	a			mnawambia
			n		ka		m	gamb	ir	a		ga	nilikwisha mwambia
			ch					zil		e			kimekuja
			e										
			a	ka	e			lum		a			Amejiuma
	ka		ba	ta			n	kom	er	a	yo		Wasinifungie huko
	m		ba					beg	es	a	ho		Wanawa- fundishia hapo

2.2 Matokeo ya irabu ishilizi

Kuna matokeo ya aina mbili ya irabu ishilizi (*-ir-e*, na *-e*) katika mazingira yafuatayo kama yanavyojibainisha pia katika Luhaya (Rubanza 1988) na Runyambo (Rugemalira 2005) :

- wakati timilifu *-ir-e* :
bazin-ir-e waliimba (k.m. jana)
ba-a-zin-ir-e walikwisha imba (siku zilizopita)
- katika muunganiko wa dhamira agizi na kiambishi awali:
chi-kol-e kifanye
ba-lek-e waache

- mfuatano wa nyakati pamoja na ukanushi:
ti-ba-k-ombekil-e hawajajenga
ti-ba-ka-swil-e hawajaoa

2.3 Tangamano irabu katika mnyambuliko wa kitenzi

Lugha ya Luzinza, kama zilivyo lugha nyingi nyinginezo za Kibantu, inadhahirisha minyambuliko ya aina mbalimbali na yenye umuhimu tofauti. Minyambuliko hii inabainishwa katika viambishi tamati vinavyofungamanishwa kwenye mzizi wa kitenzi. Mfungamanisho huo wa viambishi fuatishi huongeza na/au kurekebisha maana ya kitenzi kinachofungamanishwa na viambishi hivyo. Hili tutalieleza kwa kirefu katika sehemu zinazofuata. Katika kipengele hiki tunaelezea maumbo ya tangamano irabu yanayojitokeza kama inavyojidhahirisha katika lugha nyingi za Kibantu cha Mashariki (Rugemalira, 2005) kwa msingi wa kanuni ya tangamano irabu kati ya mzizi na upanuzi wa viambishi fuatishi.

<i>-baaga</i>	<i>-baag-ir-a</i>	<i>-baag-is-a</i>	chinja
<i>-runga</i>	<i>-rung-ir-a</i>	<i>-rung-is-a</i>	tia viungo
<i>-jimba</i>	<i>-jimb-ir-a</i>	<i>-jimb-is-a</i>	vimba, umuka
<i>-tela</i>	<i>-tele-er-a</i>	<i>-tel-ez-a</i>	piga
<i>-loga</i>	<i>-log-er-a</i>	<i>-log-es-a</i>	loga

Ukichunguza kwa makini mifano hiyo utaona kuwa matokeo ya irabu yanategemea irabu zilizomo kwenye mzizi. Ikiwa mzizi una irabu /a-u-i/ irabu tangamano inakuwa [-i-] na ikiwa mzizizi /e na o/ inakuwa irabu [-e-]. Utaratibu huo unaweza kukanunishwa ifuatavyo:

$$i \xrightarrow{\text{Mzizi}} i/\{MZ\} \xrightarrow{\{a-u-i\}} \text{___} \xrightarrow{e/} \text{___}$$

Kanuni hii inaeleza kuwa irabu [-i-] inajitokeza kama [-i-] ikiwa ndani ya mzizi kuna irabu [-a-, -u-, -i-] na inajitokeza kama [-e-] mahali penginepo. Hali hiyo inadhahirisha kuwa utokeaji wa irabu unategemea mwinuko wa ulimi. Irabu za juu na ya chini [i, u, na a] husababisha utokeaji wa irabu za juu [i na u] kama yalivyo katika maneno *-baaga* chinja *runga* tia viungo na *jimba* vimba na irabu [e] hutokea mahali penginepo yaani irabu zilizomo katika mzizi {e na o} kama katika maneno *-tela* piga na *loga* loga. Hata hivyo mizizi yenye silabi moja inajibainisha tofauti kama ioneshwavyo katika mifano ya jedwali la 2.

Jedwali la 2: Tangamano irabu fuatishi katika vitenzi vya silabi moja (KI)

Kifasiri	Kitenzi	Mzizi	-ir-	-is-
kuwa	kisoukomo <i>kuha</i>	-h-	-heera	-hiisa

kufa	<i>kufa</i>	-fu-	-feera	-fiisa
kuanguka	<i>kugwa</i>	-gu-	-gweera	-gwiisa
kula	<i>kurya</i>	-ri-	-riira	-riisa
ku(m)pa	<i>kuhe</i>	-he-	-heera	-hiisa
kusa	<i>kusa</i>	-se-	-seera	-siisa
kucha	<i>kuce</i>	-ce-	-ceera	-ceisa
kunywa	<i>kunywa</i>	-nyo-	-nyeera	-nyeisa
kumaliza	<i>kuhwa</i>	-ho-	-weera	_____

Jedwali hili linaonesha kuwa, kwa mfano, mzizi wa kitenzi wenye irabu [-u-] *-fu-* unajitokeza na irabu [-e-] (*-heera*) badala ya kujitokeza kama **fiira* kama kanuni inavyodai.

2.4 Viambishi tangulizi

Kielezo kinachofuata kinaonesha viambishi awali (mofimu tangulizi) vinavyotokea kabla ya mzizi:

Jedwali la 3: Mfuatano wa viambishi tangulizi

Kba/sh/kan1	Kn*	Kan2	Nj*	Kan2	Kb-uk	kan	Krj/yb**	MZ
n-+/ti-	-ta-	-ta-	ku	-ta-	-kwi-	-lim-
1/2/3	4	5	6	7		5	8	9

- Kba: Kiambishi awali
- Sh: Sharti
- Kan1: Kanushi (ti-)
- Kn: Kiambishi nafsi
- Kan2: Kanushi 2 (-ta-)
- Nj: Njeo
- Kb-uk: Kiambishi kitenzi kisoukomo (ku-)
- Krj : Kiambishi rejeshi
- Yb: Yambwa+

Maelezo:

- (i) Uteuzi wa kiambishi awali huelekeza uteuzi wa kiambishi nafsi lakini si kinyume chake
- (ii) ** humaanisha mfuatano wa kipashio husika kimoja au zaidi
- (iii) Hutokea kiambishi nafsi kanushi kimoja katika kitenzi
- (iv) Alama ya + ina maana kuwa kiambishi husika kina maumbo mbalimbali

Ingawa si lengo letu kueleza kwa ukamilifu viambishi vyote vya kitenzi itafaa angalau kutaja baadhi, ambavyo ni pamoja na:

- i) Viambishi vya nafsi
- ii) Viambishi vya njeo

- iii) Viambishi vya hali
- iv) Viambishi virejeshi

Mfano wa viambishi vya nafsi ni kama vinavyooneshwa katika kielelezo cha 3.

Jedwali la 3. Viambishi vya nafsi

Nafsi	Katika nafasi ya kiima	tafsiri	Katika nafasi ya Yambwa	tafsiri
1. umoja	<i>ni-som-a</i>	ninasoma	<i>mba-m-pa</i>	wananipa
1. wingi	<i>n-tu-soma</i>	tunasoma	<i>mba-tu-ha</i>	wanatupa
2. umoja	<i>no-soma</i>	unasoma	<i>mba-ku-ha</i>	wanakupa
2. wingi	<i>ni-mu-soma</i>	mnasoma	<i>mba-ba-ha</i>	wanawapa
3. umoja	<i>na-soma</i>	anasoma	<i>mba-mu-ha</i>	wanampa
3. wingi	<i>ni-ba-soma</i>	wanasoma	<i>mba-ba-ha</i>	wanawapa

Katika sehemu hii tutaeleza kwa ufupi sana viambishi vinavyoambatanishwa na mzizi kuunda shina. Hapa tutaonesha kiambishi kimoja cha dhamira dhahiri (Kihore na wenzake 2001 katika Kiswahili) yaani-**a**, kama kwa mfano katika maneno:

- i) *fulul-a*, hamisha, *homagul-a*, bomoa
- ii) *z-a* enda, *it-a* toa roho/ua

Kwa sababu ya umuhimu wa *njeo na hali* katika vitenzi vya lugha za kibantu, Luzinza ikiwa lugha mojawapo, tunaonesha viambishi mbalimbali vya njeo za lugha hii katika Jedwali la 4:

Jedwali la 4: Mfumo wa njeo na hali katika kitenzi cha Luzinza

Njeo	Yakinishi		Kanushi		Maelezo
	Umoja	Wingi	Umoja	Wingi	
	ninanua	tunanunua	sinunui	hatununui	
Mwu	<i>n-teka</i>	<i>tu-teka</i>	<i>ti-n-teka</i>	<i>Ti-tu-teka</i>	-pika
Mwuu	<i>ninteka</i>	<i>ntuteka</i>	<i>ti-n-ku-teka</i>	<i>ti-tu-ku-teka</i>	
Wt	<i>n-aa-tek-ir-e</i>	<i>tw-aa-tek-ire</i>	<i>ti-n-ka-tek-ire</i>	<i>ti-tu-ka-tek-ire</i>	
Wu	<i>n-aa-teka</i>	<i>tw-aa-teka</i>	<i>ti-n-aa-teka</i>	<i>ti-tw-aa-teka</i>	
Wu2	<i>n-tek-ire</i>	<i>tu-tek-ire</i>	<i>ti-n-tek-ire</i>	<i>ti-tu-tek-ire</i>	
Wu3	<i>n-ka-teka</i>	<i>tu-ka-teka</i>	<i>ti-ndi-tek-ire</i>	<i>ti-tu-li-tek-ire</i>	
Wum	<i>n-ka-ba-n-teka</i>	<i>tu-ka-ba-tu-teka</i>	<i>n-ka-ba-n-ta-teka</i>	<i>tu-ka-ba-tu-ta-teka</i>	
Wtp1	n-da-tek-ire	Tu-ra-tek-ire	ti-n-ka-teka-ga	ti-tu-ka-tek-a-ga	Sijawahi kupika
Wtp2	n-ka-ba-nda-tek-ire	tu-ka-ba-tu-ra-tek-ire	n-ka-ba-n-ta-ka-tek-a-ga	tu-ka-ba-tu-ta-ka-tek-a-ga	
Wu	n-daa-teka	tu-raa-teka	?	?	Wakati

					ujao
Wuk	Ni-n-ja kuteka	tu-raa-teka	ti-ndi-teka?	ti-tu-ri-teka	Wakati wa ujao
Wum					Wakati wa mbali ujao
Sd	na-ku-teka	tw-a-kuteka	ti-na-ku-teka	ti-tw-a-ku- teka	

Wum: Wakati uliopo mazoea

Wus: Wakati uliopo unaoendelea

Wt: Wakati Timilifu

Wu: Wakati uliopo mazoea

Wu1: Wakati ujao 1

Wu2: Wakati ujao 2

Wu3: Wakati ujao 3

Wum: Wakati uliopita mazoea

Wtp1: wakati uliopita timilifu

Wtp2: wakati uliopita timilifu wing?

Wuk: Wakati ujao wa karibu

Wub: wakati ujao wa mbali

Sd: Sharti dhanifu

2.5 Mzizi

Katika lugha ya Luzinza kama zilivyo lugha nyinginezo za Kibantu, mzizi ni kipashio kidogo cha kilesika katika kitenzi. Tunaweza kutumia fasili ya Driever (1976:23) wakati alipofasili maana ya mzizi katika lugha ya Kiswahili ambayo nayo ni lugha mojawapo ya Kibantu. Driever alisema kuwa “ ni sehemu ya maelezo ya kitenzi ambayo hufungamana na maana ya kileksika ya kitenzi na haiwezi kufafanuliwa kimofolojia katika kiwango cha chini bila kupoteza maana.” (Tafsiri ni yangu). Mifano ya sehemu ya maneno ambayo haibadiliki ni:

- i) *-f-a/-fw-a~f-eel-a* “-fa, f-i-a”,
- ii) *-zal-a, zal-il-a, zal-w-a* “zaa, zalia (mahali, au kwa faida ya mtu/kitu)
- iii) *-zaan-a~zaan-il-a, zaan-is-a* “cheza, chezea, chezeshi”
- iv) *-twal-a~twal-il-a* “chukua, chukulia (mtu kitu)

Mifano iliyoorodheshwa katika namba tatu inaonesha kuwa licha ya mzizi kutobadilika, kuna aina mbalimbali ya mizizi kama ioneshwavyo katika mfano wa uoneshwavyo hapa chini:

- i) *-K- -ny-a, -nyw-a* enda haja kubwa, kunywa k.m maziwa

- ii) - KIK -*nob-a, -lis-a* chukia, chungu (ng'ombe)
- iii) -KIIK -*ziik-a,* ziika

2.6 Mnyambuliko wa Kitenzi

Unyambulishaji ni upakaji wa viambishi kwenye mzizi ili kuunda maneno mapya. Katika lugha ya Luzinza kitenzi kinaundwa na mzizi (MZ) pamoja na viambishi nyambulishi (Vny). Tunaweza kukanunisha mfuatano huo kama ifuatavyo:

MZ-Vny+-

Mfuatano huo huambatana na viambishi dhamira au viambishi tamati.

Viambishi nyambulishi ni pamoja na:

- i) sababishi (-ish-)
- ii) tendea (-tda-)
- iii) tendewa (-w-)
- iv) iv) tendeana/tendana (-an-)
- v) tendeka (-tdk-)
- vi) tendua (-tdu-)
- vii) uradidi

Sababishi:

- i) *sib-a* “andika” *sib-is-a* “andikisha”
- ii) *akasibisa amazina gabo* “aliandikisha majina yao”
- iii) *nogol-a* “kata” *nogo-z-a* “katisha”
- iv) *akanogozu omujenyi omuti* “alimlazimisha mgeni akate mti”

Tendwa:

- i) *loot-a* “ota” *loot-w-a* “otwa”
- ii) *omuyanda akalotwa ise* “mtoto aliotwa na baba yake”
- iii) *byal-a* “panda(k.m. mbegu)” *byal-w-a* “pandwa”
- iv) *ebijanjala bikabyalwa omuseeza* “maharage yalipandwa na mwanamme”

Tendeana/Tendana

- i) *bon-a* “ona” *bon-an-a* “onana”
- ii) *ababembe bakabonana* “Wakoma walionana”
- iii) *teel-a* “piga” *teel-an-a* “pigana”
- iv) *abachigaji bakateelana* “Vijana walipigana”

Tendeka

- i) *bon-a* “ona” *bon-ek-a* “onekana”

- ii) *mjinjiwe yaboneka* “mpenzi wake ameonekana”
- iii) *omweji gukaboneka* “mwezi ulionekana”

Tendea

- i) *leeta* “leeta” *leet-el-a* “letea”
- ii) *omukaji akaletela omuchigaji eihuha* “mwanamke alimletea kijana ua”
- iii) *f-a* “-fa” *f-i-a* “-fia”
- iv) *embwa ekafela omuchibila* “mbwa alifia msituni”

Tendua

- i) *fundula* funua *fundikira* funika
- ii) *koma* funga *komolora* fungua

Uradidi

Uradidi ni kipengele kingine kinachojitokeza katika lugha hii ni uradidi ambapo sehemu ya neno au neno lote hurudiwa. Ikiwa sehemu ya neno ndiyo inayorudiwa mchakato huo huitwa *uradidi nusu* na ikiwa neno lote linarudiwa basi mchakato huo huitwa *uradidi kamili*. Katika lugha hii tumeshindwa kupata mifano ya uradidi nusu. Mifano ifuatayo inaonesha uradidi kaili:

- i) *tela* piga *telatela* pigapiga
- ii) *zana* cheza *zanazana* chezacheza
- iii) *seka* cheka *sekaseka* chekacheka

Hali hii ya uradidi humaanisha/hutilia mkazo jambo ikiwa ni pamoja na urudiaji wa jambo hilo, utokeaji wa mara kwa mara, utokeaji wa mfululizo au utokeaji wa nguvu.

Dhana ya kutendua katika lugha hii si zalishi na hivyo imetolewa mifano bila maelezo ya kina. Mifano ya ziada ni pamoja na ifuatayo:

- i) *-haba* kosea (k.m. njia), *-habula* sahihisha (k.m. pata njia sahihi)
- ii) *-sona* shona, *-sonolora* shonoa.

2.7 Maana za jumla za minyambuliko

Kwa jumla minyambuliko hiyo iliyotajwa hapo juu ni kama ioneshwavyo katika jedwali la 5:

Jedwali la 5: Baadhi ya maana za minyambuliko

Na.	Aina ya mnyambuliko	Maana ya mnyambuliko	Maumbo ya mnyambuliko	Mifano
1.	Sababishi	Hali ya kitu au mtu kufanya kitu	-is-, -vy-, -z-, -y-	<i>-gwa</i> anguka, <i>gwisa</i> angusha, <i>lekela</i> acha, <i>lekeza</i> achisha
2.	Tendwa/tendea	Ni kueleza hali ya kutendwa au kutendewa	-w-,	<i>-ziika,</i> zika, <i>ziikwa,</i> ziikwa, fukia kitu/maiti
3.	Tendena/Tendeana	Tendo kufanywa pamoja na kitu/mtu kufanyiana	-angan-, -an-	<i>bona</i> ona, <i>bonangana</i> onana, <i>zenda</i> nenda, <i>zendanwa</i> neanda pamoja
4.	Tendeka	Hali ya uwezekano wa kutendeka jambo	-ek/ik-,	<i>henda,</i> vunja, <i>hendeka,</i> vunjika
5.	Tendea	Huelezea mnufaishwa, lengo au sehemu	-el/-il-,	<i>hingula</i> pita, <i>hingulila</i> pitia, <i>henda</i> vunja, <i>hendeka</i> vunjika
6.	Tendua	Hali ya kufanya kinyume jambo	-ul-,	<i>-haba</i> kosea (k.m. njia), <i>habula</i> sahihisha (k.m. oneshwa njia sahihi)
7.	uradidi	Hali inayodhihirisha urudiaji wa jambo, au utokeaji wa mara kwa mara.	-iliz/-elez, -aaj-, na -ul-	

3. Hitimisho

Makala hii ililenga kutoa vidokezo vya mofolojia ya kitenzi katika lugha ya Luzinza. Hii ni hatua ya awali itakayotwezesha kuandika kwa kina kiasi ya Luzinza. Tunakaribisha maoni ambayo yatatuwezesha kufanya utafiti wa ziada ili kukamilisha kazi hii na kuwa mchango mmojawapo wa hazina ya lugha za Tanzania.

Marejeo

Guthrie, M. (1948) *The classification of Bantu languages*. London: Oxford University Press.

http://www.bantu-languages.com/en/bantu_intro.html 22/4/html. 22/04/2009.

<http://www.orvillejenkins.com/profiles/zinza.html> 4/23/2009

Kihore, Y.M. na wenzake (2001) *Sarufi ya Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D. (2000) "Ciruari Verbal Inflection" katika *Languages of Tanzania*, Kahigi, K. na wenzake, Leiden.

Nurse, D. (1979) *Description of Sample Bantu Languages of Tanzania*. *African Languages*, 5 (1), kur.1-50.

Nurse and Phillipson (wah.) (1980) *The Bantu languages*. London: Curzon Press.

Polome, E.C. (1976) *Swahili Language Handbook*. Washington D.C.: Centre for Applied Linguistics.

Rubanza, Y.I. (1988) *Linear order in Haya Verbal Morphology: Theoretical implications*. Ph.D. Dissertation. Michigan State University. East Lansing, Michigan, USA.

Rubanza, Y.I. (2008) *Msamiati wa Luzinza-Kiswahili- Kiingereza na Kiingereza-Luzinza-Kiswahili. Lexicon Series. No. 8*. Dar es Salaam: Lot Publications.

Rugemalira, J.M. (2005) "A Grammatical Sketch of Runyambo." katika *Occasional Papers in linguistics*. Dar es Salaam: LOT Publications, kur. 38-75.